

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

650

HAIBA NA MICHEZO

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi kazi mbili kwa kila aina ya tathmini zifuatazo;
 - (a) Tathmini Awali
 - (b) Tathmini endelevu
2. Katika kufanya maandalizi ya andalio la somo, mwalimu anapaswa kuzingatia sifa zipi muhimu ili kuandaa lengo mahsusi bora? Bainisha sifa nne.
3. Afisa Elimu Wilaya amekuomba uandae wasilisho la mada kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi kwa walimu wakuu. Fafanua kwa kifupi hoja nne utakazoandaa na kuziwasilisha.
4. Katika mkutano na mkuu wa chuo, baadhi ya wanachuo walitoa hoja kuwa ufundishaji kiduchu unawapotezea muda wao wa kujisomea. Hata hivyo, wewe ulikuwa na maoni kuwa ufundishaji huo ni muhimu. Bainisha hoja nne kwa kifupi kutetea msimamo wako.
5. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa kifupi umuhimu wa matumizi ya vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
6. Ukiwa ni mwalimu wa somo la Haiba na Michezo, bainisha viashiria vinne vinavyoonesha kuwa mwanafunzi ameathirika kutokana na kuishi katika mazingira magumu.
7. Tatizo la upungufu wa zana za kufundishia na kujifunzia linaweza kutatuliwa kwa njia ya kufaragua zana. Eleza kwa kifupi stadi nne anazotakiwa kuwa nazo mwalimu ili aweze kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia.
8. Fafanua kwa kifupi mambo manne ambayo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anapaswa kuyazingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.
9. Ainisha zana nne anazohitaji mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya Azimio la Kazi na kwa kila moja bainisha matumizi yake.
10. Umeteuliwa kuwa kwenye jopo litakalohusika na uteuzi wa vitabu vya kiada vya masomo mbalimbali. Eleza kwa kifupi vigezo vinne vya kuzingatia wakati wa kuchagua kitabu cha kiada kwa ajili ya somo la Haiba na Michezo.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali manne (4) kutoka sehemu hii.

11. "Mhutasari wa somo ni muhimu kwa walimu wageni lakini siyo kwa walimu wazoefu." Kanusha usemi huo ukionyesha madhara matano ya kufundisha bila kuwa na mhutasari wa somo.
12. Eleza kwa ufasaha mambo matano yanayoweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba ya wanafunzi.
13. Kwa kutumia hoja tano, fafania mambo ya kuzingatia ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
14. Eleza kwa ufasaha namna mwalimu anavyopaswa kutumia vipengele vitano vya andalio la somo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
15. Fafania vipengele vitano vya Azimio la Kazi ambavyo hutumika wakati wa maandalizi ya Andalio la somo la Haiba na Michezo.
16. "Shajara ni mojawapo ya nyaraka muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo." Kwa kutumia hoja tano, thibitisha kauli hii.